# MTIHANI WA KUTATHMINI WA MENTOR - 2021
# DARASA LA 8
# KISWAHILI (LUGHA) **(002)**

**Muda:** Saa 1 dakika 40

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI**

1.Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu kina maswali 50.

2.Ukiisha kuchagua jibu lako, lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha kwamba umeandika yafuatayo katika karatasi ya majibu.

**NAMBA YAKO YA MTIHANI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE YAKO**

5. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani(yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzoni mwa karatasi ya majibu.
6. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
7. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
8. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C. D.Ni jibu **MOJA tu** kati ya hayo manne ambalo ni sahihi.Chagua jibu hilo.
9. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

Katika kijitabu cha maswali:

**20.** Bainisha matumizi ya 'karibu' katika sentensi: **Ameanguka karibu avunjikee mguu.**

A. Makaribisho
B. Kiasi
C. Nusura
D. Wakati

Jibu sahihi ni C

**Katika karatasi ya majibu:**

1. [A] [B] [C] [D] 10. [A] [B] [C] [D] 20. [A] [B] [C] [D] 30. [A] [B] [C] [D] 40. [A] [B] [C] [D]

katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 20, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

10. Chora kistari chako vizuri.Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
11. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**GEÚZA UKURASA**

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo chini. Chagua lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa kujaza kila pengo.***

Ushirikiano ______1_____ ya wanafunzi, walimu na wazazi ni jambo _____2______ _____3_____ maanani na wahusika wote. ______4_____ huleta mafanikio hasa ya wanafunzi wenyewe. Aidha, hukuza ______5_____ ya kiheshima. ______6_______ akabiliwapo na matatizo, hukumbushwa ya wahenga kuwa ______7______ kwani wenzake humfaa kwa hali na mali.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **1.** A. baina | B. kati kati | C. miongoni | D. kati |
| **2.** A. linalohitajika | B. inayohitajika | C. inaohitajika | D. yanayohitajika |
| **3.** A. kutia | B. kutilia | C. kutiliwa | D. kutiwa |
| **4.** A. Hiyo | B. Huu | C. Huo | D. Ule |
| **5.** A. maadili | B. maarifa | C. maoni | D. nasaha |
| **6.** A. Lolote | B. Yeyote | C. Yoyote | D. Wowote |

**7.** A. mazoea yana taabu  B. chanda chema huvishwa pete
C. mkataa wengi ni mchawi  D. ndugu mui heri kuwa naye.

_______8______ maisha yangu ya _______9_______, taswira ya mwalimu Busara hunijia. Ndiye aliyechangia katika ______10_______ kwangu masomoni. ______11______ wake katika somo la Kiswahili uliniwezesha kutumia kamusi ipasavyo. Akasisitiza kuwa kati ya maneno: shtaka, somea, sinia na sebule; linalopatikana la tatu katika kamusi ni ______12______. Katika sarufi, akatubainishia kuwa kutokana na kitenzi "vumilia" tunapata "uvumilivu" ambalo ni ______13_______. Pamoja na ukarimu wake, nilijifunza msemo wa kuwa na ______14______ . Kweli, bwana Busara asingalikuwepo _____ 15_____ hayo yote muhimu.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **8.** A. Nikiyakunjua | B. Nikikunjua | C. Nikiyakunja | D. Nikikunjika |
| **9.** A. baadaye | B. usoni | C. leo | D. kisogoni |
| **10.** A. mafanikio | B. fanaka | C. kufanikiwa | D. ufanisi. |
| **11.** A. Ubunifu | B. Ustadi | C. Uungwana | D. Uzalendo |
| **12.** A. sebule | B. sinia | C. somea | D. shtaka |
| **13.** A. nomino | B. kitenzi | C. kivumishi | D. kielezi |
| **14.** A. mkono birika | B. mkono mzuri | C. mkono wazi | D. mkono mrefu. |
| **15.** A. nisingalijifunza | B. nisingejifunza | C. ningejifunza | D. ningalijifunza |

**<u>Kutoka swali la 16 - 30, chagua jibu sahihi.</u>**

**16.** Chagua neno lenye sauti **ghuna**.

A. Chupa B. Maradhi
C. Thelathini D. Mshumaa.

**17.** Maria akigawa robo mara mbili sawia, atapata akisami gani?

A. Sudusi B. Robo mbili
C. Thumni D. Nusu.

**18.** Sentensi gani **<u>sahihi kisarufi</u>**?

A. Watume walioleta nyaraka walichelewa kufika.
B. Mishumaa yaliyonunuliwa yalitumika yote.
C. Mlolongo wa magari yalifuatana .
D. Vijana walishambuliwa na viboko maziwani.

**19.** Ni jibu lipi lenye maelezo **sahihi**?

A. Utaya ni nyama zinazoshika meno kinywani.
B. Kipaji ni sehemu ya mbele ya kichwa.
C. Kitanga ni sehemu ya vidole.
D. Muundi ni sehemu ya mguu iliyo baina ya goti na kiuno.

**20.** Kundi lipi lenye nomino katika ngeli ya **U-U** pekee?

A. Unga, uteo
B. Umaskini, uyoga
C. Umma, ubavu
D. Uzi, uta

**21.** Orodha ipi inalingana?

A. Tarbia, malenga, ngonjera
B. Kibwagizo, vina, takhmisa
C. Utenzi, ngonjera, tathlitha.
D. Ukwapi, utao, manju.

**22.** Chagua sentensi yenye **<u>na</u>** ya kuonyesha mtendaji.

A. Anahisi maumivu ya kichwa.
B. Susana na Batu ni wanafunzi watiifu.
C. Uandishi umefundishwa na mwalimu stadi.
D. Mheshimiwa ana gari jibya.

**23.** Chagua sentensi **iliyoakifishwa ipasavyo**?

A. Lo? Nani alikuruhusu kuyanywa maji ambayo hayajachemshwa?
B. Lo, nani alikuruhusu kuyanywa maji ambayo hayajachemshwa?
C. Lo! Nani alikuruhusu kuyanywa maji ambayo hayajachemshwa.
D. Lo! Nani alikuruhusu kuyanywa maji ambayo hayajachemshwa?

**24.** Chagua viambishi vya nafsi kwenye neno '**<u>tunakujalia</u>**'?

A. na - ja
B. li - a
C. tu - ku
D. na - li

**25.** Ni jibu lipi lenye **<u>vielezi</u>** pekee?

A. sote, chenyewe, popote, kwenye
B. sana, nadra, safi, vyema.
C. kiasi, mno, ajabu, asubuhi.
D. leo, baadaye, laini, laiti.

**26.** Kauli: Nekesa na Hadija wameandikishwa insha na mwalimu wao ni **<u>sawa</u>** na kusema:

A. Nekesa na Hadija wameandika insha kwa niaba yao.
B. Mwalimu wao amewaandikia Nekesa na Hadija insha.
C. Nekesa na Hadija wameandika insha kwa niaba ya mwalimu wao.
D. Mwalimu wao amewafanya Nekesa na Hadija kuandika insha.

**27.** Methali "Fimbo ya mbali haiui nyoka" huambiwa anayetegemea walio mbali kutatulia matatizo yake. Je, asiyejua namna na mikakati bora zaidi ya kutekeleza jambo huambiwa?

A. Makaa hayaoki nyama
B. Kisu kibutu hakichinji kuku
C. Jina la sifa huletwa na matendo
D. Chombo imara hustahimili mawimbi makali.

**28.** Chagua jibu linalounganisha sentensi hizi mbili inavyofaa:
**Mvua ilinyesha kidindia. Wakulima hawakupanda mapema.**

A. Mithili ya mvua kunyesha kidindia, wakulima hawakupanda mapema.
B. Mvua ilinyesha kidindia lau wakulima hawakupanda mapema.
C. Wakulima hawakupanda mapema madhali mvua ilinyesha kidindia.
D. Licha ya mvua kunyesha kidindia, wakulima hawakupanda mapema.

**29.** Chagua jibu **lisilolingana** na mengine.

A. Buda - ajuza
B. Kiambaza - ukuta.
C. Panga - pangua
D. Mavyaa - bavyaa.

**30.** Andika katika usemi wa taarifa: "Je, tarakilishi hutumiwa katika mawasiliano?" Mwanafunzi akasema.

A. Mwanafunzi aliulizwa ikiwa tarakilishi hutumiwa katika mawasiliano.
B. Mwanafunzi alitaka kujua iwapo tarakilishi hutumiwa katika mawasiliano.
C. Mwanafunzi aliomba kueleza matumizi ya tarakilishi.
D. Mwanafunzi alitaka kujua je, tarakilishi hutumiwa katika mawasiliano.

***Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali 31 - 40.***

Makuzi ya watoto hutegemea sana jamii yenye msimamo thabiti katika suala hili. Hoja ya wazazi isiwe tu kujitafutia mali ovyo bali iwe ni ya kutambua warithi wa mali inayosakwa. Hii ndiyo sababu wazazi wengi leo hujikusuru kuisimamisha misingi ya malezi bora ya watoto kwa kuwasomesha.

Kumsomesha mtoto tu bila msingi wa nidhamu ni kama kulijenga jumba la ghorofa bila msingi imara na **kuporomoka kwake si ajabu**. Vijana wanapaswa kuelewa umuhimu huu ili wawe tayari kuupokea uongozi na urathi wa jamii.

Misingi madhubuti ya kinidhamu hujengwa tangu watoto wakianza kutambua mambo. Kumngoja hadi mtoto awe mkubwa ndipo aanze kufunzwa maadili ni kama kujaribu kuuwahi udongo ukiwa **umekauka na kuwa mkavu**; samaki mkunje angali mbichi.

Hapo zamani mambo yalikuwa tofauti. Mtoto aliweza kukosolewa na mtu yeyote hata kama alikuwa mpita-njia. Watoto walikuwa ni wa jamii, hulka zao zilionekana mapema. Watoto walikuwa wakitenda mambo huku wakijihisi kuwa jamii imewakodolea macho.

Hisia hizo ziliwafanya kujichunguza, kujikosoa na kutenda mambo kwa tahadhari. Waliwaheshimu watu wazima bila masharti hali ambayo ilikuza uhusiano bora katika jamii.

Mtoto afunzwaye adabu ipasavyo kawaida **hawezi kutetereka** popote alipo, iwe shuleni au nyumbani. Mtoto kama huyo kufanywa **kuwa bendera inayofuata upepo** na watovu wa nidhamu sio rahisi, bali atachukua nafasi ya walimu na wazazi kuyapitisha maadili yafaayo kwa wenzake. Mtoto huyo hukuza mbegu bora katika jamii. Wazazi wakilea watoto wa aina hii na wawaongezee mafunzo ya kidini, jamii itakuwa na uhakika wa kuwa na urithi bora. Watoto hao wataweza kuchangia pakubwa katika maendeleo ya nchi kwa jumla.

Kuna haja sasa ya kufuata tamaduni na itikadi za kigeni katika maisha. Tukome ubaguzi, uvivu na ubinafsi ili kuwapa watoto mifano bora na miangaza ya kuwakuza kifikira, kielimu, kiuchumi na kitamaduni. Jamii izidishe michango yake katika urekebishaji wa watoto.

**Watoto nao wana jukumu la kuyaimarisha maisha yao.** Wanapaswa kuziepuka tabia zote mbaya hata kama hawapewi misingi makwao. Wanaweza kuyatupilia mbali maovu ambayo yanawazunguka katika jamii. Wakumbuke kuwa urithi bora ni ule wa kuiga tabia njema, jitihada na kupata elimu yenye manufaa.

---

**31.** Kulingana na kifungu, misingi bora ya watoto hukuzwa kwa:
- A. Wazazi kutotafuta mali ovyo na kuwasomesha warithi.
- B. Kuujua umuhimu wao na kuwapa maelekezi.
- C. Kuwa na misingi madhubuti shuleni
- D. Kufunza watoto kujikusuru kiuchumi.

**32.** Maana ya "**kuporomoka kwake si ajabu**" ni:
- A. Haijalishi kuwa ghorofa litaporomoka.
- B. Malezi ya watoto kuharibika si kazi.
- C. Wazazi kushindwa na malezi si jambo la kustaajabisha.
- D. Si vigumu jamii kupoteza warithi.

**33.** **Umekauka na kuwa mkavu;** huweza kulinganishwa na:
- A. Madhara ya uchelewashaji wa kufunza nidhamu.
- B. Ugumu wa malezi bora.
- C. Madhara ya ucheleweshaji wa masomo ya watoto.
- D. Ugumu wa kuwakosoa watoto.

**34.** Kulingana na ufahamu, watoto wa zamani:
- A. Walikuzwa vigumu.
- B. Waliwaogopa wazazi wao.
- C. Walikomaa kwa haraka.
- D. Walikuzwa kwa ushirikiano.

**35.** Watoto kuhisi kuwa jamii inawakodolea macho, kuliwafanya waweze:
- A. Kuithamini jamii zaidi
- B. Kuiogopa jamii majumbani
- C. Kuwajibika katika jamii.
- D. Kurekebisha tabia katika jamii.

**36.** Kauli "**<u>....... kuwa bendera inayofuata upepo</u>**" inamaanisha:

A. Mtoto mwenye nidhamu kufuatwa na watovu wa nidhamu.

B. Matendo maovu kumfuata mtoto mwenye nidhamu.

C. Kawaida ya bendera kufuatana na upepo.

D. Mtoto mwenye nidhamu kufuata matendo ya waovu.

**37. Watoto nao wana jukumu la kuyaimarisha maisha yao.** Methali inayoweza kujumuisha kifungu hiki ni:

A. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.

B. Mtoto akibebwa hutazama kisogo cha nina.

C. Ukibebwa usilevyelevye miguu.

D. Wimbo mui hauimbwi mwana.

**38.** Warithi bora katika jamii hukuzwa kwa:

A. Malezi bora na elimu.

B. Kuheshimiwa na wakubwa.

C. Malezi ya kizamani.

D. Kuaminiwa na jamii.

**39.** Maana ya "**<u>hawezi kutetereka</u>**" ni:

A. Hawezi kubabaika

B. Hawezi kupotoka

C. Hawezi kushawishika

D. Hawezi kutetemeka.

**40.** Kichwa mwafaka kwa taarifa hii ni:

A. Urithi wa jamii bora

B. Msingi wa jamii bora

C. Majukumu ya malezi.

D. Bendera hufuata upepo.

***<u>Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali 41-50.</u>***

Tuliongoza mifugo yetu hadi malishoni. Ulikuwa ni msimu wa kiangazi nalo jua lilikuwa kali. Sote tulikuwa maghulamu wa hirimu moja. Kiranja wetu alikuwa na umri wa miaka kumi na mitatu.

Baada ya kuichunga mifugo kwa saa mbili hivi, tuliamua kwenda kuogelea katika dimbwi lililokuwa kitalifa kifupi kutoka hapo machungani. Ilibidi tuiache mifugo pale mikononi mwa mmoja wetu. Hakuna aliyejitolea kubaki. Sote tulitaka kwenda kuogelea.

Lisilobudi hubidi. Tulikata shauri kupiga kura. Tulipiga kura na Musa akawa ndiye angeichunga mifugo. Tuling'oa nanga kwa vicheko huku tukimwacha Musa katika hali ya huzuni na upweke. Tulimpa pole za bandia huku tukimcheka kisirisiri. Wengine walisikika wakimtania kuwa wangempelekea maji aogelee pale malishoni wakati wa kurejea. **<u>Laiti tungalijua yaliyotungojea!</u>** Kwa mara ya kwanza nilijigeuza kuwa maji yafuatayo mkondo. Niliyatemea mate maonyo ya mamangu.

Tuliandamana na wenzangu moja kwa moja kuelekea dimbwini. Kabla hatujafika, tuliamua kupitia shambani mwa mzee Kaumu. Konde lake lilijaa mihogo. Tuliivamia kwa uroho uliopita ule wa fisi.

Dakika chache baadaye, tulikuwa njiani kuelekea dimbwini tayari kuogelea. Ungetusikia ungesamehewa iwapo ungedhani ni kundi la fisi kutokana na vicheko na mbwembwe zetu.

Tulifika dimbwini na kuanza kuogelea. Kila samaki alitaka kudhihirisha ubingwa wake. Tulipiga mbizi kwa ustadi mkuu. Wengine kama mimi, tulijirushia rushia maji kandokanda ya dimbwi. Mtu hujikuna ajipatapo. Au niseme ukimwiga tembo kunya utapasuka msamba. Nilidhamiria kurejea kiamboni nikiwa mzima.

Hata wanagenzi kama mimi, baadaye tulitekwa bakunja na uogeleaji. **Tulipotanabahi giza lilikuwa likibisha hodi.** Mbiombio tulielekea tulipoziweka nguo zetu. La ajabu hata Musa alikuwa kati yetu. Hakuna aliyemwuliza mbona akaja au ilikokuwa mifugo kwani maajabu mengine yalitukodolea macho. Nguo zetu hazikuwepo. Mungu mwema! Tuliangaliana bila kusema lolote.

Tukiwa katika hali ya kuchanganyikiwa, tulisubiri hadi giza lilipotanda kabisa. Kumbuka wahenga walisema usiku ni lebasi bora. Tulifika manzilini baada ya safari ya tahadhari kuu kupitia vichakani.

Kiamboni nilikuta mengine. Mmiliki wa shamba la mihindi lililopakana na malishoni alikuwa pale machozi yakimdondoka. Mazao yake yote yalikuwa yameangamizwa na mifugo yetu. Vilevile, mzee Kaumu alikuwa pale akililia damu yetu. Kumbe tayari alikuwa ameiuza mihogo ile ! Angemwelezaje mteja wake? Yaliyonipata jioni hiyo mikononi mwa mama, sidhani yatafutika akilini mwangu hadi gharighari ya mauti yangu. Kwa njia moja au nyingine yalikuwa ni **dira** ya maisha yangu. La sivyo, labda leo hii nisingethaminiwa katika jamii.

---

**41.** Kwa nini wahusika walishiriki upigaji kura?
- A. Walitaka kuenda kuogelea.
- B. Walikuwa na nia ya kumchagua kiranja.
- C. Walikuwa wamekosa kukubaliana yupi kati yao angebaki na mifugo.
- D. Walikosa kiongozi atakayewaongoza.

**42.** Kulingana na ufahamu, ni kweli kusema kuwa:
- A. Wahusika wote walifurahia matokeo ya kura.
- B. Msimulizi hakufurahia matokeo ya kura.
- C. Wenzake Musa walimtania.
- D. Musa alifurahia matokeo ya kura.

**43.** Tabia ya msimulizi inaweza kujumuishwa kuwa:
- A. Utundu na utukutu
- B. Utiifu na uwajibikaji
- C. Uzembe na mabezo
- D. Uaminifu na ukarimu.

**44.** Kulingana na aya tano, **si kweli** kusema:
- A. Musa na wenzake walipitia shamba la mzee Kaumu kabla ya kufika dimbwini
- B. Msimulizi na wenzake hawakufululiza moja kwa moja hadi dimbwini.
- C. Wahusika walifurahia uogeleaji.
- D. Msimulizi na wenzake waliingiwa na tamaa.

45. Kauli "**Laiti tungalijua yaliyotungojea ...**" inaweza kujumuishwa kwa methali gani :

A. Pilipili usioila yakuwashiani?
B. Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki.
C. Mzigo u kichwani kwapa latokeani jasho?
D. Jambo usilolijua ni kama usiku wa kiza.

46. Kulingana na kifungu, mzee Kaumu alichelea nini hasa?

A. Mihogo yake kuharibiwa na mifugo.
B. Kufidia hasara ya mihogo.
C. Kupata hasara ya mihogo.
D. Kuwaadhibu msimulizi na wenzake

47. Sentensi: "**Tulipotanabahi giza lilikuwa likibisha hodi**" imetumia fani gani?

A. Msemo
B. Methali
C. Uishi
D. Kinaya.

48. Mpangilio upi unaonyesha mfuatano mwafaka wa matukio katika taarifa?

*i. Ng'ombe kuangamiza mazao ya mmiliki wa shamba la mahindi*
*ii. Kuliwazia tendo la ukaidi*
*iii. Kupiga kura*
*iv. Msimulizi kukaidi ushauri wa mama yake.*

A. iii, iv, i, ii
B. i, ii, iii, iv
C. iv, iii, i, ii
D. ii, iii, iv, i

49. Tendo linaloonyesha kutowajibika kwa msimulizi ni:

A. Kuandamana na wenzake malishoni
B. Kujaribu kujifundisha kuogelea
C. Kuamua kupiga kura
D. Kuwafuata wenzake kwenda kuogelea.

50. Neno "**dira**" kama lilivyotumika katika aya ya mwisho linamaanisha:

A. Mustakabali
B. Kifaa cha kuelekeza msafiri
C. Mafunzo
D. Maarifa.